

## **Mpango wa Kupanua Usikivu Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)**

Katika bajeti ya Maendeleo TBC imekuwa ikipatiwa fedha na Serikali kwa ajili ya upanuzi wa Usikivu wa redio ambao umeongezeka kutoka asilimia 55 mwaka 2016 hadi asilimia 63 mwaka 2018.

Aidha, katika bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka 2019/2020 TBC itatekeleza miradi ya upanuzi wa Usikivu kwenye mikoa ya Njombe, Simiyu, Songwe pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba upande wa Tanzania Zanzibar. Kukamilika kwa mradi huu kutawezesha TBC kufikia usikivu wa asilimia 73.